

## **FURSA SAWA NI SHERIA**

Ni kinyume cha sheria kwa mpokeaji huyu wa msaada wa kifedha wa Serikali kubagua kwa misingi ifuatayo: dhidi ya mtu yeyote nchini Marekani, kwa misingi ya uraia, rangi, dini, jinsia (ikijumuisha ujauzito, uzazi, na hali zinazohusiana na matibabu, ubaguzi wa kijinsia, hali ya kubadilisha jinsia, na utambulisho wa kijinsia), asili ya kitaifa (ikijumuisha ustadi mdogo wa Kiingereza), umri, ulemavu, au ushirika wa kisiasa au imani, au, dhidi ya mnufaika yeyote wa, mwombaji, au mshiriki katika mipango inayosaidiwa kifedha chini ya Title I ya Sheria ya Uvumbuzi na Fursa ya Kazi, kwa misingi wa hali ya uraia ya mtu binafsi au ushiriki katika mpango au shughuli yoyote inayosaidiwa kifedha ya WIOA Title I-

Mpokeaji hapaswi kubagua katika mojawapo ya maeneo yafuatayo: kuamua ni nani atayekubaliwa, au ataweza kupata programu au shughuli yoyote ya WIOA Title I-yenye msaada wa kifedha; kutoa fursa, au kushughulikia mtu yeyote kuhusiana na mpango au shughuli kama hiyo; au kufanya maamuzi ya ajira katika uwasilishaji, au kuhusiana na mpango au shughuli kama hiyo.

Wapokeaji wa msaada wa kifedha wa serikali ni lazima wachukue hatua nzuri ili kuhakikisha kuwa mawasiliano na watu wenye ulemavu ni sawa na mawasiliano na watu wengine. Hii ina maana kuwa, wapokeaji wanahitajika kutoa misaada na huduma zinazofaa kwa watu walemavu waliostahiki wanapombwa kufanya hivyo na bila gharama yoyote kwa mtu huyo.

### **UNAPASWA KUFANYA NINI IKIWA UNAAMINI UMEBAGULIWA**

Ikiwa unafikiria kuwa umekabiliwa na ubaguzi chini ya mpango au shughuli ya WIOA Title I-inayosaidiwa kifedha, unaweza kuwasilisha malalamiko ndani ya siku 180 kutoka tarehe ya ukiukaji unaodaiwa kwa: Afisa wa Fursa Sawa wa mpokeaji (au mtu ambaye ameteuliwa na mpokeaji kwa kusudi hili);

**AU: Mkurugenzi, Kituo cha Haki za Kiraia (CRC), Marekani. Idara ya Kazi**  
**200 Constitution Avenue NW, Chumba cha N-4123, Washington, DC 20210**  
au kwa njia ya kielektroniki kama ilivyoelekezwa kwenye tovuti ya CRC katika [www.dol.gov/crc](http://www.dol.gov/crc).

Ikiwa utawasilisha malalamiko yako kwa mpokeaji, ni lazima usubiri hadi mpokeaji atoe Ilani iliyoandikwa ya Hatua ya Mwisho, au hadi siku 90 ziwe zimepita (ile itakayokuwa mapema), kabla ya kuwasilisha katika Kituo cha Haki za Kiraia (tazama anwani iliyo hapo juu). Ikiwa mpokeaji hatacupa Ilani iliyoandikwa ya Hatua ya Mwisho ndani ya siku 90 kufuatia siku ambayo uliwasilisha malalamiko yako, unaweza kuwasilisha malalamiko kwa CRC kabla ya kupokea Ilani hiyo. Hata hivyo, ni lazima uwasilishe malalamiko yako ya CRC ndani ya siku 30 za tarehe ya mwisho ya siku 90 (kwa maneno mengine, ndani ya siku 120 baada ya siku ambayo uliwasilisha malalamiko yako kwa mpokeaji). Ikiwa mpokeaji atakupatia Ilani iliyoandikwa ya Hatua ya Mwisho kuhusu malalamiko yako, lakini haujaridhishwa na uamuzi au suluhisho, unaweza kuwasilisha malalamiko kwa CRC. Ni lazima uwasilishe malalamiko yako ya CRC ndani ya siku 30 baada ya tarehe ambayo ulipokea Ilani ya Hatua ya Mwisho.

Idara ya Kazi ya Vermont ni mwajiri na mtoa huduma anayetoa fursa sawa kwa wote. Ikiwa una ulemavu na unahitaji msaada wa habari hii, tafadhali piga simu kwa 7-1-1 ili kupata Huduma ya Relay ya Vermont. Tafadhali piga simu kwa 802-828-4000 na ubonyeze 0 ili kuomba habari isiyo ya malipo kwa muundo mbadala, ikijumuisha tafsiri ya lugha unayopendelea.